



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

BARAZA LA FAMASI



TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI WA MALALAMIKO DHIDI YA MITIHANI YA USAJILI NA TAALUMA KWA KADA YA FAMASI

Dodoma; Aprili 17, 2025

Tarehe **03 Aprili, 2025**, Baraza la Famasi lilitoa matokeo ya mitihani ya Usajili na taaluma iliyofanyika tarehe 19 – 21 Februari, 2025. Mitihani hiyo ilihusisha Wafamasia, Fundi Dawa Sanifu, Fundi Dawa Wasaidizi na Watoa dawa wa Mwaka Mmoja (*Medicine dispensers*).

Baraza linawajibika kisheria kusimamia taaluma ya famasi na utendaji wa wanataaluma nchini ikiwa ni pamoja na kuwasajili baada ya kufuzu mitihani ya taaluma ambayo inaendeshwa kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Famasi, Sura 311. Mitihani inayoratibiwa na Baraza la Famasi ni mahususi kwa ajili ya kupima umahiri wa wahitimu kabla ya kusajiliwa kama inavyofanyika kwa mabaraza na taaluma nyingine za afya nchini na duniani.

Baada ya matokeo ya mitihani ya Februari 2025 kutolewa, yamekuwepo malalamiko kwenye mitandao ya kijamii hususan kuhusu matokeo yaliyowahusu Fundi Dawa Sanifu. Malalamiko hayo yalijikita zaidi katika kuonesha kuwa mitihani ya taaluma inawanyima haki watahiniwa hasa wale ambao hawakufaulu mitihani hiyo.

Hivyo basi, Baraza la Famasi lingependa kutoa ufafanuzi kwa umma hasa wale ambao wanahisi wameathrika na matokeo ya mitihani ya mwezi Februari 2025 kama ifuatavyo;

- a) Kiwango kidogo cha ufaulu kwa watahiniwa licha ya kuwa wamehitimu na kupatiwa mafunzo ya kina kwa muda wa miaka mitatu.**

Baraza la Famasi linapenda kufafanua kuwa lengo la mitihani hii ni kupima umahiri na uwezo wa muhitimu kutoa huduma za dawa ikiwemo kwa wagonjwa. Baraza linaisitiza watahiniwa kujiandaa vema na kutilia mkazo mafunzo kwa vitendo (*field work*) ambayo yanalenga kumpa mwanafunzi uzoefu na weledi wakati wa kutoa huduma za dawa. Baraza linashauri mafunzo haya yatiliwe mkazo ili kila mwanafunzi apate ujuzi wa kutoa huduma za afya kama vile kutoa huduma za dawa kwa

wagonjwa katika viwango vya kitaaluma na kulinda afya za wananchi.

b) Madai ya kukosekana kwa uwazi katika utungaji na usahihishaji wa mtihani, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa *marking scheme* ya wazi na ya kueleweka kwa wanaotarajiwa kufanya mtihani

Baraza linapenda kufafanua kuwa, kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya uendeshaji wa mitihani ya aina yoyote, zoezi la uendeshaji wa mitihani ya taaluma kuanzia utungaji hadi kutolewa kwa matokeo ni la siri. Aidha zoezi husika hushirikisha wanataaluma kutoka taasisi mbalimbali na vyombo vingine vya Serikali ili kuimarisha ubora wa mitihani na utunzaji wa siri wakati na baada ya mitihani.

c) Matokeo ya mitihani kutokuwa ya haki

Baraza la Famasi limeweka utaratibu unaozingatia haki za mtahiniwa kuanzia wakati wa kuomba kufanya mitihani, kufanya mitihani, kusahihisha na kutoa matokeo. Kila mtahiniwa hupewa namba ya mtihani na humiliki akaunti binafsi katika mfumo wa *Pharmacy Council Management Information System (PCMIS)* ambao hutumiwa katika mawasiliano na mtahiniwa ikiwa ni pamoja na matokeo yake.

Kadhalika, Baraza limeweka utaratibu maalum wa kuwasilisha maoni ya kutokuridhishwa na matokeo na maelekezo/ushauri kwa mtahiniwa ambaye hajaridhika na matokeo yake kuwa ana haki ya kuomba mtihani wake usahihishwe tena. Hivyo, endapo kuna mtahiniwa anahisi hakutendewa haki, anayo nafasi ya kusikilizwa na kuomba mtihani wake usahihishwe upya.

d) Baraza la Famasi kutokusahihisha mitihani iliyofanyika badala yake wanapanga idadi ya watu wanaotakiwa kufaulu

Baraza linapenda kufafanua kuwa, mitihani yote inafuata taratibu za mitihani ikiwemo kusahihishwa kabla ya matokeo kutolewa. Utaratibu wa usahihishaji wa mitihani hujumuisha wanataaluma walioteuliwa kutoka katika Wizara, Vyuo na taasisi mbalimbali za kiutendaji ndani ya Serikali. Hivyo, mtihani wa kila mtahiniwa, ikiwemo ile iliyofanyika mwezi Februari 2025, husahihishwa na jopo la wataalamu na wasimamizi wengine na kisha kuhakikiwa kabla ya matokeo kutolewa.

e) Kutokufahamika kwa alama za ufaulu wa mitihani ya taaluma

Alama za ufaulu wa mtihani wa Usajili na taaaluma zipo wazi na zimeainishwa kwenye mwongozo wa Mitihani ya Taaluma na Usajili wa mwaka 2019, kipengele cha 7 (C) kinachoeleza kuwa mtahiniwa anapaswa kupata ufaulu wa angalau asilimia sitini (60%)

kwa kila mtihani. Mwongozo huo unapatikana katika tovuti ya Baraza la Famasi kwa ajili ya kila mwananchi wakiwemo watahiniwa kuupitia na kuona alama za ufaulu.

Hitimisho

Mitihani ya taaluma na usajili ni muhimu kwa lengo la kuhakikisha wanataaluma wanaosajiliwa wanakidhi viwango vya kitaluuma vinavyosimamiwa na Baraza katika utendaji wa taaluma ili kulinda afya za wananchi kupitia huduma watakazozitoa. Aidha, Baraza linashirikiana na mamlaka za ithibati katika kupata ufumbuzi wa changamoto zinazopelekea ufaulu hafifu ili kuimarisha viwango vya ufaulu kwa wanataaluma wa famasi na hivyo kuimarisha huduma za dawa na afya kwa ujumla katika jamii.

Imetolewa na:



Boniface M. Magige
MSAJILI
BARAZA LA FAMASI